

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA DAR ES SALAAM**

Anwani ya Simu:  
Simu: 2203156/58  
Fax: +25522203213  
Tovuti: [www.dsm.go.tz](http://www.dsm.go.tz)  
Barua Pepe: [ras@dsm.go.tz](mailto:ras@dsm.go.tz)



**OFISI YA MKUU WA MKOA**  
**3 Barabara ya Rashidi**  
**Kawawa,**  
S.L.P 5429,  
**12880 -DAR ES SALAAM.**  
**Tanzania**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**MKUU WA MKOA MHE. PAUL MAKONDA AKABIDHIWA DOUBLE CABIN WINGLE 5.**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam **Mhe. Paul Makonda** leo asubuhi amekabidhiwa zawadi ya gari aina ya **Double Cabin Wingle 5** kutoka kwa kampuni ya watengenezaji wa magari ya **Great Wall Motor** ya Afrika Kusini ikishirikiana na kampuni ya wauzaji wa magari ya **Kifaru Motors** ya Tanzania.

Akiongea katika makabidhiano hayo Mkurugenzi wa **Great Wall Motor Company** ukanda wa kusini mwa Afrika **Bwana Jianguo Liu** alisema kuwa zawadi hiyo ni ishara ya kampuni hiyo kutambua jitihada mbalimbali za Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na watumishi wake wanazofanya katika kutumikia wananchi na kusaidia kuboresha utendaji kazi.

Katika salamu za shukrani **Mhe. Paul Makonda** aliushukuru Uongozi mzima wa Kampuni ya **Great Wall Motor** ukishirikiana na wauzaji wa magari ya **Kifaru Motors** kwa kutambua jitihada za Ofisi yake na kuahidi kuendelea kuwatumikia wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa moyo na kutimiza falsafa ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Dkt. John Pombe Magufuli** ya **“HAPA KAZI TU”**.

Mkuu wa Mkoa ameahidi kuwa gari hilo litatumika ipasavyo katika kuwahudumia wananchi wa Dar es Salaam na kutumiwa na Idara itakayoonekana kuwa ndio mtoa huduma bora katika Mkoa wa Dar es Salaam.

***“Naomba kuitoa hii gari kama zawadi kwa Idara inayohudumia vizuri wananchi wangu na ili nitoe kwa Idara hiyo naomba wananchi wenyewe watutumie kwa ujumbe mfupi kupitia namba tutakayoitangaza. Kazi ya wananchi ni kusema tu Idara hii inawahudumia vizuri wanapofika kwenye ofisi zao, kama ni Afya, Elimu, Ardhi, Biashara, na Mahakama”***. Aliongeza **Mhe. Paul Makonda**.

Kwa mfano kama ulienda Idara ya Elimu, Ardhi, Afya, au Biashara ukapewa huduma nzuri katika eneo mojawapo kati ya hayo unachotakiwa kufanya ni kutuma mesesji fupi inayoonyesha Idara hiyo ili wapewe zawadi hiyo ya Gari kama motisha ili waendeleo kutoa huduma nzuri.

Utaratibu wa kutuma ujumbe huo wa kuchagua Idara bora katika utendaji utatolewa kupitia namba maalum ambayo itatolewa hapo baadae.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

**OFISI YA MKUU WA MKOA**

**DAR ES SALAAM**

05/07/2017